*"Enyi watu wangu, sikieni mafundisho yangu, sikilizeni maneno ya kinywa changu. Nitafumbua kinywa changu kwa* ***mafumbo,*** *nitazungumza mambo yaliyofichika, mambo ya kale, yale ambayo tuliyasikia na kuyajua, yale ambayo baba zetu walituambia. Hatutayaficha kwa watoto wao tutakiambia kizazi kijacho matendo yastahiliyo sifa ya BWANA,"*(Zaburi 78:1-4).

**Kutimia**

*"Yesu alinena mambo haya yote kwa makutano kwa mifano. Wala pasipo mfano hakuwaambia lo lote. Hii ilikuwa ili kutimiza lile lililonenwa kwa vinywa vya manabii kusema: ''Nitakifungua kinywa changu niseme nao kwa mifano, nitahubiri mambo yaliyofichika tangu kuumbwa kwa misingi ya ulimwengu''* (Mathayo 13:34-35).



**Unabii wa Ishirini na Mbili wa Biblia**
**Masihi alikuwa aiingie hekaruni.**

Reproduction, resale or internet posting prohibited

"*Angalieni, nitamtuma mjumbe wangu, atakayeiandaa njia mbele yangu. Ndipo ghafula Bwana mnayemtafuta atakuja hekaluni mwake. Mjumbe wa agano, ambaye mnamwonea shauku, atakuja,'' asema BWANA Mwenye Nguvu" (*Malaki 3:1).

**Kutimia**

*"Yesu alipoingia Yerusalemu, mji wote ukatataharuki, watu wakauliza, "Huyu ni nani?'' Ule umati wa watu ukajibu, "Huyu ni Yesu, yule nabii kutoka Nazareti katika Galilaya.'' Yesu akaingia katika eneo la hekalu na kuwafukuza wote waliokuwa wakinunua na kuuza vitu hekaluni, akazipindua meza za watu waliokuwa wakibadilisha fedha na viti vya wale waliokuwa wakiuza njiwa*"(Mathayo 21:10-12).



**Unabii wa Ishirini na Tatu**

**Masihi alikuwa aingie Yerusalemu kwa punda.**

*"Shangilia sana, Ee Binti Sayuni! Piga kelele, Binti Yerusalemu! Tazama, mfalme wako anakuja kwako, ni mwenye haki naye ana wokovu, mpole naye amepanda punda, mwana punda, mtoto wa punda*"(Zekaria 9:9).

Hii ilikuwa unabii wa kushangaza. Wafalme hawakuwa wanaingia kwa vita juu ya punda, lakini kila mara wakiwa juu ya farasi mweupe.

Yesu watu walifikiri kwamba Yesu atakuja kwa Yerusalemu kuleta "ulimwengu mpya"ama ufalme wake.



Ukweli ufalme huu wa kwanza Yesu alipanda juu ya punda akiingia Yerusalemu. Lengo lake lilikuwa kuleta ufalme wa kiroho kwa kushinda adui yake ya kiroho shetani.Alifanya hivyo wakati aliruhusu shetani, kupitia watu wamsulubishe.

Wakati wa pili Yesu atakuja Yerusalemu atakuwa na farasi nyeupe kwa sababu atakuwa mfalme na Mungu wa Miungu!

Reproduction, resale or internet posting prohibited



"*Kisha nikaona mbingu imefunguka na hapo mbele yangu akiwepo farasi mweupe, ambaye Yeye aliyempanda huyo farasi aliitwa Mwaminifu na wa Kweli. Yeye ahukumu kwa haki na kupigana vita" (Ufunuo 19:11)*

**Kutimia**



*"Walipokuwa wanakaribia Yerusalemu, wakafika Bethfage katika Mlima wa Mizeituni, ndipo Yesu akawatuma wanafunzi wake wawili, akiwaambia, "Ingieni katika kijiji kilichoko mbele yenu, nanyi mtakuta punda amefungwa na mwanapunda pamoja naye. Wafungueni na mniletee. Kama mtu ye yote akiwasemesha lo lote, mwambieni, 'Bwana ana haja nao, naye atawaruhusu mwalete mara. Haya yalitukia ili litimie lile lililonenwa na nabii, akisema:*

*''Mwambieni Binti Sayuni, 'Tazama, mfalme wako anakuja kwako, ni mnyenyekevu, naye amepanda punda, juu ya mwanapunda, mtoto wa punda.' Wale wanafunzi wakaenda, wakafanya kama vile Yesu alivyokuwa amewaagiza. Wakamleta yule punda na mwanapunda, nao wakatandika mavazi yao juu ya hao punda na Yesu akaketi juu yake"* (Mathayo 21:1-7).

Reproduction, resale or internet posting prohibited

**Unabii wa Ishirini na Nne**

**Masihi atakuwa kizuizi kwa wayahudi,na wengi watamkataa.**

***“****Kwa hiyo hivi ndivyo BWANA Mwenyezi asemavyo: “Tazama, ninaweka jiwe katika Sayuni, jiwe lililojaribiwa, jiwe la pembe la thamani kwa ajili ya msingi thabiti, yeye atumainiye kamwe hatatiwa hofu”* (Isaya 28:16).

***“****Jiwe walilolikataa waashi,limekuwa jiwe kuu la pembeni,*” (Zaburi 118:22).

“*Alidharauliwa na kukataliwa na wanadamu, mtu wa huzuni nyingi, ajuaye mateso. Kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao alidharauliwa, wala hatukumhesabu kuwa kitu*”(Isaya 53;3).

**Kutimia**



***“****Kwa maana Maandiko yasema: “Tazama, naweka katika Sayuni, jiwe la pembeni, teule lenye Thamani na kila amwaminiye hataaibika.” Kwenu ninyi mnaoamini, Yeye ni wa thamani. Lakini kwao wasioamini, “Jiwe lile walilolikataa waashi limekuwa jiwe kuu la pembeni,” tena, “Jiwe lenye kuwafanya watu wajikwae, mwamba wa kuwafanya waanguke.” Wanajikwaa kwa sababu hawakutii lile neno, kama walivyowekewa tangu zamani*” (1pet 2:6-8).

“Hapo mwanzo, alikuwako Neno. Huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu” (Yohana 1:11).

Reproduction, resale or internet posting prohibited

Yesu alikuja kama amenyenyekea na mpole kwa huu ulimwengu.Wengi wa Wayahudi na wengi wa enzi zake. Walikuwa wana mwangazia mtu aliyekaa kufanikiwa kwa macho yao ya kidunia. Watu wengi hawawezi kuamini Masihi ni Mungu.Wakati atakapokuja mara ya pili atakuja kama mfalme anayetawala!

Watu huona kama hii wazo la Masihi kuwa Mungu linaharibu maandiko ile inasema “*Sikia, Ee Israeli: BWANA Mungu wako, ni BWANA mmoja*”(Kumbukumbu 6:4).

Ukweli nyumaye kama uumbaji , Mungu alifanya ajulikane kama “SISI na NASI”

***“****Ndipo Mungu akasema, “Tufanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu, wakatawale juu ya samaki wa baharini na ndege wa angani, juu ya mifugo, juu ya dunia yote, na juu ya viumbe wote watambaao juu ya nchi*”(Mwanzo 1:26).

*“Hapo mwanzo Mungu aliumba mbingu na dunia” (*Mwanzo 1:1).*Neno ambalo limetumika la Mungu katika maandiko haya ni “Elohim” linahidhilisha Mungu katika hali ya Wingi.*

Biblia inatufunza kwamba Mungu ako na umbo tatu lakini ni Mungu mmoja.Yeye hujitokeza na kufanya kazi wakati mwingine kama Baba, Roho, na wakati mwingine kama Mwana wa Mungu ama kwa maneno Mengine kama Neno lake Mungu.

**Unabii wa Ishirini na Tano**

**Masihi atakuwa nuru kwa Watu wengi wa Mataifa**

**"***Anasema: "Je, ni jambo dogo sana wewe kuwa mtumishi wangu ili kurejeza upya makabila ya Yakobo, na kuwarudisha wale Waisraeli niliowahifadhi. Pia nitakufanya uwe nuru kwa ajili ya Mataifa, ili upate kuleta wokovu wangu hata miisho ya dunia*"(Isaya 49:6).

Tangu mwanzo Mungu alimchangua Ibrahimu ili kuaazisha Familia Ambayo Yesu atazaliwa. Ibrahimu awakawa Waebrania,au mwazisha wa familia ya Mungu. Katika ya Karne kadhaa Waebrania alijihisi Mungu ni Mungu wao pekee au Muyahudi.



Ukweli nikuwa Mungu alitumia Waebrania kuwa bariki Wayahudi,kwa jina linguine mataifa. Katika Mwanzo 12:1-3, Mungu alimwambia Ibrahimu yakuwa atambariki,ili familia zote za dunia zi barikiwe. Mpango wa Mungu ulikuwa kubariki watu wote wa ukoo na ukombozi wake.

Katika kitabu cha Amosi Mungu alinena na Wayahudi, na maandiko mengi.

***"Katika siku ile nitaisimamisha hema ya Daudi iliyoanguka. Nitakarabati mahali palipobomoka na kujenga upya magofu yake na kujenga kama ilivyokuwa awali, ili wapate kumiliki mabaki ya Edomu na mataifa yote yale yanayobeba jina langu,'' Asema BWANA ambaye atafanya mambo haya"(*Amosi 9:11,12).

**Kutimia**

Reproduction, resale or internet posting prohibited



*"Ndipo Paulo na Barnaba wakawajibu kwa ujasiri, wakisema, 'Ilitupasa kunena nanyi neno la Mungu kwanza. Lakini kwa kuwa mmelikataa, mkajihukumu wenyewe kuwa hamstahili uzima wa milele, sasa tunawageukia watu Mataifa.Kwa maana hili ndilo Bwana alilotuamuru: " 'Nimewafanya ninyi kuwa nuru kwa watu Mataifa, ili mpate kuuleta wokovu hadi miisho ya dunia.' " Watu Mataifa waliposikia haya wakafurahi na kulitukuza neno la Bwana, nao wote waliokuwa wamekusudiwa uzima wa milele wakaamini*"(Matendo 13:46-48).

**Sehemu ya 4 - Kusulubishwa kwa Masihi na maelezo zaidi yaliyolitabiriwa katika Maandiko ya Kiyahudi**

**Unabii wa Ishirini na Sita wa Biblia**
**Masihi atasalitiwa na Rafiki yake.**

*"Hata rafiki yangu wa karibu, niliyemwamini, yule aliyekula chakula changu ameniinulia kisigino chake*" ( Zaburi 41:9)

Katika unabii huu inataja rafiki wakaribu, alikuwa na uhusiano wa agano na Yeye, aliye msaliti Masihi.

**Kutimia**

Hasa hii ilitendeka maishani mwa Yesu. Yuda Isakarioti mmoja wa wanafaunzi wa Yesu. Alikuwa muweka Hazina. Kusaliti kwake ni timizo la kusulubiwa kwa Yesu.

*''Sisemi kuhusu ninyi nyote. Ninawajua wale niliowachagua. Lakini ni ili maandiko yapate kutimia, 'Yeye aliyekula chakula changu, ameinua kisigino chake dhidi yangu.' ''Ninawaambia mambo haya kabla hayajatukia, ili yatakapotukia mpate kuamini kuwa Mimi ndiye*"( Yohana 13:18,19).

*"Baada ya kusema haya, Yesu alifadhaika sana moyoni, akasema, ''Amin, amin, nawaambia, mmoja wenu atanisaliti''* (Yohana 13:21).

**"***Yesu akajibu, ''Ni yule nitakayempa hiki kipande cha mkate baada ya kukichovya kwenye bakuli.'' Hivyo baada ya kukichovya kile kipande cha mkate, akampa Yuda, mwana wa Simoni Iskariote*" (Yohana 13:26)

Reproduction, resale or internet posting prohibited





*"Mara tu baada ya kukipokea kile kipande cha mkate, Shetani akamwingia. Yesu akamwambia Yuda, ''Lile unalotaka kulitenda litende haraka*" (Yohana 13:27).

*"Yesu alipomaliza kuomba, akaondoka na wanafunzi Wake wakavuka Bonde la Kidroni. Upande wa pili palikuwa na bustani, Yeye na wanafunzi Wake wakaingia humo. Basi Yuda, yule aliyemsaliti alipafahamu mahali hapo kwani Yesu alikuwa akikutana humo na wanafunzi Wake mara kwa mara. Hivyo Yuda akaja bustanini, akiongoza kikosi cha maaskari wa Kirumi na baadhi ya maafisa kutoka kwa viongozi wa makuhani na Mafarisayo, wakiwa wamechukua taa, mienge na silaha. Yesu akijua yale yote yatakayompata, akajitokeza mbele yao akawauliza, ''Mnamtafuta nani?'' Wao wakamjibu, ''Yesu wa Nazareti.'' Yesu akawajibu, "Mimi ndiye.'' Yuda, Yule aliyemsaliti alikuwa amesimama pamoja nao. Yesu alipowaambia, 'Mimi ndiye,' walirudi nyuma na kuanguka chini*!"(Yohana 18:1-6).

## Unabii wa Biblia Ishirini na Saba
## Masihi atauzwa vipande 30 vya fedha.

**"***Nikawaambia, "Mkiona kuwa ni vema, nipeni ujira wangu, la sivyo, basi msinipe.'' Kwa hiyo wakanilipa vipande thelathini vya fedha*"(Zakeria 11:12).

**Kutimia**

***"****Kisha mmojawapo wa wale kumi na wawili, yeye aitwaye Yuda Iskariote, alikwenda kwa viongozi wa makuhani na kuuliza, "Mtanipa nini nikimtia Yesu mikononi mwenu? Wakamlipa vipande thelathini vya fedha*"(Mathayo 26:14,15).



Wakati Yuda alimsaliti Yesu,alifanya hivyo kwa malipo ya vipande 30 vya fedha,bei ya mtumwa.Baadaye, Yuda alijitowa uhai mwenyewe. Hakuomba toba.

---

## Unabii wa Ishirini na Nane
## Vipande 30 vya fedha zitarejeshwa kwa mfanyizi uumbaji.

Reproduction, resale or internet posting prohibited

**"**Naye BWANA akaniambia, "Mtupie mfinyanzi,'' hiyo bei nzuri waliyonithaminia! Kwa hiyo nikachukua hivyo vipande thelathini vya fedha na kumtupia huyo mfinyanzi katika nyumba ya BWANA" (Zakeria 11:13).

**Kutimia**

***"****Yuda, ambaye ndiye aliyekuwa amemsaliti Yesu, alipoona kuwa Yesu amehukumiwa, akajuta na akarudisha vile vipande thelathini vya fedha alivyopewa na viongozi wa makuhani na wazee wa watu. Akasema, "Nimetenda dhambi, kwa maana nimeisaliti damu isiyo na hatia." Basi Yuda akavitupa vile vipande vya fedha ndani ya hekalu akaondoka akaenda na kujinyonga*"(Mathayo 27:3-5).



***"****Wale makuhani wakuu wakazichukua zile fedha wakasema, ''Si halali kuchanganya fedha hizi na sadaka kwa sababu hizi ni fedha zenye damu.'' Kwa hiyo baada ya kushauriana, waliamua kuvitumia kununulia shamba la mfinyanzi, liwe mahali pa kuzikia wageni"*(Mathayo 27:6,7).

**"***Hii ndiyo sababu lile shamba likaitwa, 'Shamba la Damu' hadi leo. Ndipo likatimia lile lililonenwa na nabii Yeremia kwamba, ''Walichukua vile vipande thelathini vya fedha, thamani aliyopangiwa na watu wa Israeli, wakanunulia shamba la mfinyanzi, kama vile Bwana alivyoniagiza.'' Wakati Yesu akiwa amesimama mbele ya mtawala, mtawala akamwuliza, "Wewe ndiye mfalme wa Wayahudi?''* (Mathayo 27:8-11).

---

## Unabii wa Ishirini na Tisa
## Mashahidi wa uongo wamstaki Masihi.

***"****Usinitie katika nia ya adui zangu, kwa maana mashahidi wa uongo wameinuka dhidi yangu, wakipumua jeuri*" ( Zaburi 27:12).

***"****Alidharauliwa na kukataliwa na wanadamu, mtu wa huzuni nyingi, ajuaye mateso. Kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao alidharauliwa, wala hatukumhesabu kuwa kitu*" (Isaya 53:3).

***"****Lakini yalikuwa ni mapenzi ya BWANA kumchubua na kumsababisha ateseke, ingawa BWANA amefanya maisha yake kuwa sadaka ya hatia, ataona uzao wake na kuishi siku nyingi*,"(Isaya 53:10).

**Kutimia**

***"****Lakini hawakupata jambo lo lote, ingawa mashahidi wengi wa uongo walijitokeza. Hatimaye wakajitokeza mashahidi wawili wa uongo na kusema : "Huyu mtu alisema, 'Nina weza kulivunja hekalu la Mungu na kuijenga tena kwa siku tatu*" (Mathayo 26:60,61).

Reproduction, resale or internet posting prohibited

Yesu hajawai tenda dhambi, au kufanya kitu kibaya. Hakuwa enda kinyume na sheria. Njia mwafaka ya maadui zake kuhidhilisha hatia Yake nikuwa na mashahidi wa uongo watakao ongea uongo kumuhusu.

Watu wa dini ya Yesu mchana wao walikuwa wamemchukia. Walitumiwa na shetani kumsulubisha. Hii ni ya ukweli hadi waleo. Wengi wanao jitabua kama wadini hawamfahamu Yesu, wala hawa mwamini Yeye.

---

## Unabii wa Biblia Thelathini
## Masihi atakuwa kimia mbele ya adui Zake.

***"****Alionewa na kuteswa, hata hivyo hakufungua kinywa chake, aliongozwa kama mwana kondoo apelekwaye machinjoni, kama vile kondoo anyamazavyo mbele ya amkataye manyoya, hivyo hakufungua kinywa chake"* (Isaya 53:7).

Kutimia



*"Lakini viongozi wa makuhani na wazee walipomshtaki, hakujibu neno. Ndipo Pilato akamwuliza, "Je, husikii ni mambo mangapi wanayokushtaki nayo?'' Lakini Yesu hakumjibu hata kwa shtaka moja,kiasi kwamba mtawala alishangaa sana*"(Mathayo 27:12-14).

*Yesu angefungua kinywa chake, angekombolewa. Maneno Yake yana nguvu yakuwa angefunja nguvu za watesi na wauaji wake. Lakini Yesu alifahamu lazima afe kwa dhambi za dunia.*

---

**Unabii wa Biblia Thelathini na Moja**

**Masihi atateseka kwa niaba ya wengine.**

*"Hakika alichukua udhaifu wetu na akajitwika huzuni zetu, hata hivyo tulifikiri amepigwa na Mungu, amepigwa sana naye na kuteswa.Lakini alitobolewa kwa ajili ya makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu, adhabu iliyotuletea sisi amani ilikuwa juu yake, na kwa majeraha yake sisi tumepona"* (Isaya 53:4,5).

Reproduction, resale or internet posting prohibited



Nabii Isaya alisema haya mika mia moja kabla Masihi haja sulubishwa. Alifahamu haya kupitia Roho wa Mungu.




Kutimia

*"Jioni ile, wakamletea watu wengi waliopagawa na pepo, naye akawatoa wale pepo kwa neno lake, na kuponya wagonjwa wote. Haya yalifanyika ili litimie lile lililonenwa kwa kinywa cha nabii Isaya kwamba:* (Mathayo 8:16, 17).

**Unabii wa Thelathini na mbili**
**Masihi alipigwa na wakamtemea mate.**

**"***Niliwapa mgongo wangu wale wanipigao, mashavu yangu wale wang'oao ndevu zangu, sikuuficha uso wangu kutokana na fedheha na kutemewa mate*" (Isaya 50:6).

*Yesu aliteseka kupindukia hata kabla haja sulubiwa msalabani. Mgongo wake ulitolewa nyama chini ya mifupa alishapwa na mjeledi uliokuwa na chuma cha pua na mifupa ikifunganishwa pande zote.*



**"***Kisha wakamtemea mate usoni na wengine wakampiga ngumi. Wengine walimpiga makofi na kusema, "Tutabirie, wewe Kristo! Ni nani aliyekupiga?" (*Mathayo 26:67, 68).

---

Reproduction, resale or internet posting prohibited

**Unabii wa Biblia Thelathini na tatu**
**Masihi ata dhihakiwa na kutusiwa.**

*"Mimi ni mnyoo wala si mwanadamu, wanaume wamenibeza na watu wamenidharau Wote wanionao hunidhihaki, hunivurumishia matusi, wakitikisa vichwa vyao.Husema, "Anamtegemea BWANA, basi BWANA na amwokoe. Amkomboe basi, kwa maana anapendezwa naye" (Zaburi 22:6-8).*

Ni jambo la muhimu kufahamu kuwa Zaburi 22 inanena jua ya na inaelezea kusulubishwa, na miaka maelfu kabla ya Warumi kutimiza jambo la kushangaza. Una weza fuata mstari iliyo katika Zaburi nautabue vile Yesu ali nukuu kuhusu kusulubiwa kwake. Maneno yake ya mwisho yalikuwa " imeisha," ni sawa na maneno ya zamani yaliyo tafsiriwa katika mstari wa mwisho wa Zaburi 22.

**Kutimia**



**"**Kisha askari wa mtawala wakampeleka Yesu kwenye Praitorio**a** na wakakusanya kikosi kizima cha askari kumzunguka. Wakamvua nguo Zake na kumvika vazi la rangi nyekundu, kisha wakasokota taji ya miiba wakaiweka kichwani pake. Wakamwekea fimbo katika mkono wake wa kuume, wakapiga magoti mbele zake na kumdhihaki wakisema "Salaam, mfalme wa Wayahudi!'' Wakamtemea mate, wakachukua ile fimbo wakampiga

kichwani tena na tena. 31Baada ya kumdhihaki, wakamvua lile vazi , wakamvika tena nguo Zake. Kisha wakampeleka ili kumsulibisha" (Mathayo 27:27-31).

Alipokuwa Yerusalemu mwaka wa 2006, Tuliona tendo Hili kwa Mathayo 27 lilipotendeka. In tendo lilifanywa na askari Warumi kama "Mchezo wa Mfalme". Mchezo uko sawa na mwingeni unaitwa(board game), lakini hii ilifanyika sakafuni. Wangeweza kumtoka mfungwa katika sehemu mmoja haki nyingine alikimtesa "mchezo wa mfalme" tendo la kumudhulumu hadi kifo. Tunapo tazama maelezo sakafuni, tunaweza kuhisi ndani ya mioyo yetu vile Yesu alivumilia mateso,na hivyo basi hakufunga mdomo wake kujiokoa.

**"***Watu waliokuwa wakipita njiani wakamvurumishia matukano huku wakatikisa vichwa vyao na kusema, "Wewe ambaye utalivunja hekalu na kulijenga kwa siku tatu, jiokoe mwenyewe basi! Kama Wewe ni Mwana wa Mungu, shuka kutoka msalabani''* (Mathayo 27:39-40).

---

**Unabii wa Biblia thelathini na nne**

**Masihi atanguka akiwa amebeba msalaba Wake.**

**"**Magoti yangu yamelegea kwa kufunga, mwili wangu umedhoofika na kukonda. Nimekuwa kitu cha kudharauliwa kwa washtaki wangu, wanionapo, hutikisa vichwa vyao"(Zaburi 109:24,25).

**Kutimia**

**"***Yesu akiwa ameubeba msalaba Wake,akatoka kuelekea mahali palipoitwa, 'Fuvu la Kichwa,' au ambapo kwa Kiebrania ni Golgotha*"(Yohana 19:17).

*"Walipokuwa wakienda naye, wakamkamata mtu mmoja aitwaye Simoni mweyeji wa Kirene, aliyekuwa anatoka shambani. Wakambebesha msalaba, wakamlazimisha auchukue nyuma ya Yesu*"(Luka 23:26).

Reproduction, resale or internet posting prohibited

Yesu alikuwa karibu kufa alipokuwa amebeba msalaba kuelekea mlimani kusulubiwa. Alikuwa amepigwa na kudhulumiwa kwa siku kadhaa. Alianguka na uzito wa msalaba, ambao Simioni kutoka Cyrene alibeba polipobaki.

---

**Unabii wa Biblia Thelathini na Tano.**

**Mikono na miguu ya Yesu itatobolewa**.

"*Mbwa wamenizunguka, kundi la watu waovu limenizingira, wametoboa mikono yangu na miguu yangu"* (Zaburi 22:16).

**Kutimia**



*"Lakini Thomasi, aliyeitwa Didimasi, yaani, Pacha, mmoja wa wale kumi na wawili, hakuwa pamoja nao Yesu alipokuja. Hivyo wale wanafunzi wengine wakamwambia, ''Tumemwona Bwana.''*

*Lakini yeye akawaambia, ''Nisipoona zile alama za misumari mikononi mwake na kuweka kidole changu kwenye hizo alama za misumari na mkono wangu ubavuni Mwake, sitaamini.'' Baada ya siku nane, wanafunzi Wake walikuwa tena pamoja ndani ya nyumba, naye Thomasi alikuwa pamoja nao. Ndipo Yesu akaja*

*milango ikiwa imefungwa na kusimama katikati yao akasema, "Amani iwe nanyi.'' Kisha akamwambia Thomasi, "Weka kidole chako hapa na uone mikono Yangu, nyosha mkonowako uguse ubavuni Mwangu. Usiwe na shaka, bali uamini tu.'' Thomasi akamwambia, "Bwana wangu na Mungu wangu!*'' (Yohana 20:24-28).

---

**Unabii wa Biblia Thelathini na sita**

**Masihi atasulubiwa pamoja na wezi.**

*"Kwa hiyo nitamgawia sehemu miongoni mwa wakuu, naye atagawana nyara pamoja na wenye nguvu,*

*kwa sababu aliyamimina maisha yake hadi mauti, naye alihesabiwa pamoja na wakosaji. Kwa kuwa alichukua dhambi za wengi, na kuwaombea wakosaji*" (Isaya 53:12).

Reproduction, resale or internet posting prohibited

**Kutimia**



"*Wanyang'anyi wawili walisulibiwa pamoja naye, mmoja kuume Kwake na mwingine kushoto Kwake*" (Mathayo 27:38).

---

**Unabii wa Biblia Thelathini na saba**

**Masihi ataombea watu walio muua Yeye.**

*"Kwa hiyo nitamgawia sehemu miongoni mwa wakuu, naye atagawana nyara pamoja na wenye nguvu,*

*kwa sababu aliyamimina maisha yake hadi mauti, naye alihesabiwa pamoja na wakosaji. Kwa kuwa alichukua dhambi za wengi, na kuwaombea wakosaji*" (Isaya 53:12).

**Kutimia**

*"Kwa sababu hii tazama nawapelekea manabii na wenye hekima na walimu. Baadhi yao mtawaua na kuwasulibisha, wengine mtawapiga mijeledi katika masinagogi yenu na wengine mtawafuatia kutoka mji mmoja hadi mji mwingine*"(Luka 23:24).



Ikiwa Yesu aliwasemehe watu walio mdhulumu na kumsulubisha, hakika atakusamehe wewe, haijalishi vile umekuwa mbaya.

Hakuna dhambi zidisha sana; hakuna mtu mbaya sana hawezi samehewa. Hakuna shinda kuu ambayo Yesu hawezi tatua.

**Uko hai, naanaweza ishi maishaini mwako katika hali unazo pitia!**

## Unabii wa Biblia Thelathini na Nane
## Masihi alidharauliwa na kukataliwa na wanadamu.

*"Alidharauliwa na kukataliwa na wanadamu, mtu wa huzuni nyingi, ajuaye mateso. Kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao alidharauliwa, wala hatukumhesabu kuwa kitu"* (Isaya 53:3).

**Kutimia**

**"***Basi ilikuwa siku ya Maandalio ya Pasaka, yapata kama saa sita hivi. Pilato akawaambia Wayahudi, "Huyu hapa Mfalme wenu!'' Wao wakapiga kelele, "Mwondoe! Mwondoe! Msulibishe!'' Pilato akawauliza, "Je, nimsulibishe Mfalme wenu?'' Wale viongozi wa makuhani wakamjibu, "Sisi hatuna mfalme mwingine ila Kaisari.'' Ndipo Pilato akamkabidhi Yesu kwao ili"* (Yohana 19:14,15).

**"***Alikuwepo ulimwenguni na ingawa ulimwengu uliumbwa kwa Yeye, haukumtambua. Alikuja kwa walio Wake, lakini wao hawakumpokea*" (Yohana 1:10-11).

Reproduction, resale or internet posting prohibited

## Unabii wa Biblia Thelathini na Tisa
## Masihi alichukiwa bila sababu.

**"***Wale wanaonichukia bila sababu ni wengi kuliko nywele za kichwa changu, wengi ni adui bila sababu, wale wanaotafuta kuniangamiza. Ninalazimishwa kurudisha kitu ambacho sikuiba"* (Zaburi 69:4).

Kutimia

**"***Lakini hii ni kutimiza lile neno lililoandikwa kwenye Torati kwamba 'Walinichukia pasipo sababu*" (Yohana 15:25).

Hata siku leo watu humchukia Yesu bila sababu.Ambaye anaowezo wakutuza maisha yao iwe hima. Ana taka waende mbinguni na wawe na uzima wa milele.anawaokowa kutoka kuzimu,hapa duniani na milele.bado wanadamu wanamchukia bila sababu.

---

### Unabii wa Biblia arubaini
### Marafiki wa Masihi watamkwepa.

**"***Rafiki na wenzangu wananikwepa kwa sababu ya majeraha yangu, majirani zangu wanakaa mbali name"* (Zaburi 38:11).

**Kutimia**

*"Kisha wakamkamata Yesu, wakamchukua wakaenda naye mpaka nyumbani kwa Kuhani Mkuu. Lakini Petro akafuata kwa mbali*" (Luka 22:54).

"*Lakini wale wote waliomfahamu, pamoja na wale wanawake waliokuwa wamemfuata kutoka Galilaya, walisimama kwa mbali wakiyatazama mambo haya*" (Luka 23:49).

Petro mwanafunzi wa Masihi wa karibu sana,alimkataa Yeye. Lakini baadaye alisamehewa na kawa mmoja wa watume. Wengi wanaojidai wafuasi wa Masihi siku hizi bado wanamonea haya. Hawataki kujitabulisha na Yeye kwa uongo wa kukosolewa.

"*Kama mtu ye yote akinionea aibu Mimi na maneno Yangu, Mwana wa Adamu atamwonea aibu mtu huyo atakapokuja katika utukufu Wake na katika utukufu wa Baba na wa malaika watakatifu*" (Luka 9:26).

Reproduction, resale or internet posting prohibited

---

### Unabii wa BibliaArobainina Moja
### Wanadamu wanao tikiza vichwa Masihi alikuwa Msalabani.

**"***Wote wanionao hunidhihaki, hunivurumishia matusi, wakitikisa vichwa vyao*" (Zaburi 22:7).

"*Nimekuwa kitu cha kudharauliwa kwa washtaki wangu, wanionapo, hutikisa vichwa vyao*" (Zaburi 109:25).


**Kutimia**

"*Watu waliokuwa wakipita njiani wakamvurumishia matukano huku wakatikisa vichwa vyao*" (Mathayo 27:39).

**Unabii wa BibliaArobainina Mbili**
**Maaskari watagawana mavazi ya Masihi kwa kipiga kura.**

**"***Wanagawana mavazi yangu wao kwa wao na nguo zangu wakazipigia kura" (*Zaburi 22:18).

**Kutimia**



***"****Maaskari walipokwisha kumsulibisha Yesu, walichukua nguo Zake wakazigawa mafungu manne, kila askari fungu lake. Ila walikubaliana wasilichane lile vazi Lake kwa maana lilikuwa halina mshono bali limefumwa tangu juu hadi chini. Wakaambiana, "Tusilichane ila tulipigie kura ili kuamua ni nani alichukue.'' Hili lilitukia ili Maandiko yapate kutimizwa yale aliyosema, "Waligawana nguo zangu na mavazi yangu wakayapigia kura.'' Hayo ndiyo waliyoyafanya wale maaskari" (*Yohana 19:23,24).


Reproduction, resale or internet posting prohibited

---

**Unabii wa BibliaArobainina Tatu**
**Masihi atapewa divai na siki pale msalabani.**

**"***Waliweka nyongo katika chakula change na walinipa siki nilipokuwa na kiu*" (Zaburi 69:21).

**Kutimia**



**"***wakampa Yesu divai iliyochanganywa na nyongo ili anywe, lakini alipoionja, akakataa kuinywa*" (Mathayo 27:34).


Nyongo na Divai nimchanganyiko uliyo tumiwa hasa kupunguza uchungu wakati wa kusulubiwa.Yesu hakukubaliana nayo.

**Unabii wa BibliaArobainina Nne**

**Masihi atalilia Mungu Mbona umeniacha.**

*"Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha? Kwa nini uko mbali hivyo kuniokoa? Mbali hivyo na maneno ya kuugua kwangu*?" (Zaburi 22:1).

**Kutimia**



*"Ilipofika saa tisa Yesu akapaza sauti akalia, "Eloi, Eloi lama sabakthani?'' Maana yake, "Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?''* (Mathayo 27:46).

Yesu alikuwa na uhusiano wa karibu na Mungu baba alipokuwa hapa duniani. Iihali Yesu alihitajika kulipa deni yetu uliyokuwa umetanganishwa na Mungu, na njia mwafaka ni Mungu baba amuacha Yesu. Kumuacha kwa harisi. Ilituweze kuunganika na Mungu.

*Ahadi Zake kwetu ni, "Yalindeni maisha yenu msiwe na tabia ya kupenda fedha, bali mridhike na vile mlivyo navyo, kwa sababu Mungu amesema, "Kamwe sitakuacha wala sitakupungukia*" (Waebrania 13;5).

Reproduction, resale or internet posting prohibited

**Unabii wa BibliaArobainina Tano**
**Hakuna Mfupa wa Masihi utavunjika.**



"*huhifadhi mifupa yake yote, hata mmoja hautavunjika*" (Zaburi 34:20).

**Kutimia**

*"Kwa hiyo maaskari wakaenda wakavunja miguu ya mtu wa kwanza aliyesulibiwa pamoja na Yesu na yule mwingine pia. Lakini walipomkaribia Yesu, wakaona ya kuwa amekwisha kufa, hivyo hawakuvunja miguu Yake. Badala yake mmoja wa wale maaskari akamchoma mkuki ubavuni na mara pakatoka damu na maji. Mtu aliyeona mambo hayo ndiye aliyetoa ushuhuda, nao ushuhuda wake ni kweli. Anajua kuwa anasema kweli, naye anashuhudia ili pia nanyi mpate kuamini. Kwa maana mambo haya yalitukia ili Maandiko yapate kutimia, yale yasemayo, "Hakuna hata mfupa Wake mmoja utakaovunjwa''* (Yohana 19:32-36).

Ilikuwa ni desturi kuhalakisha kifo cha wale waliosulubishwa kwa kuvunja miguu yao, hasa ikiwa siku ifuatayo ni siku takatifu, ukitazama wakati wa Yesu.Wakati huu kulikuwa na sikukuu ya Pasaka. Lakini Yesu alikuwa ameshaa kufa kwa Mioyo iliyovunjika.


**Kama miaka maelfu halipo awali** Musa aliwapatia wana Waisraeli maagizo ya Pasaka., yakuwa hawapasi kuvunja mifupa ya kondoo aliyeuliwa. Ukweli ni kuwa Yesu alikuwa Kondoo la Pasaka. Kama vile damu ya Pasaka iliwazingira Wana Waisraeli kutoka kwa adui zao wakiroho, hivyo ndivyo damu ya Yesu iliwazingira kwa muovu shetani. Itawapa uzima wa milele, uzima uliyo zidi wakati wanapoishi duniani.

Reproduction, resale or internet posting prohibited

**Unabii wa BibliaArobainina Sita**
**Moyo wa Masihi utadungwa na kuvunjika.**

*"Dharau zimenivunja moyo na nimekata tamaa, nimetafuta wa kunihurumia, lakini sikumpata ye yote, wa kunituliza, lakini sikumpata ye yote*" (Zaburi 69:20).

*"Nimemiminwa kama maji, mifupa yangu yote imetoka katika viungo vyake. Moyo wangu umegeuka kuwa nta, umeyeyuka ndani yangu*" (Zaburi 22:14).



**Kutimia**

*"Badala yake mmoja wa wale maaskari akamchoma mkuki ubavuni na mara pakatoka damu na maji*" (Yohana 19:34).

Maji na damu ya Yesu ni hidhilisho kamili kuwa Yesu alikuwa amecha kufa. Alikufa kwa ajili ya moyo iliyovunjika.

Reproduction, resale or internet posting prohibited

**Unabii wa BibliaArobainina Saba**
**Masihi atachomwa ubavu Wake.**

*"Nami nitamiminia roho ya neema na maombi juu ya nyumba ya Daudi na wakazi wa Yerusalemu. Watanitazama mimi, Yule waliyemchoma, nao watamwombolezea kama mtu anayemwombolezea mwanawe wa pekee na kusikitika kwa uchungu kama anayemsikitikia mzaliwa wake wa kwanza wa kiume"* (Zekaria 12:10).

**Kutimia**

*"Badala yake mmoja wa wale maaskari akamchoma mkuki ubavuni na mara pakatoka damu na maji"* (Yohana 19:34).

*"Tena Maandiko mengine yanasema, "Watamtazama Yeye waliyemchoma kwa mkuki.''*
(Yohana 19:37).

**Unabii wa Biblia wa Arobaini na Nane**
**Kutakuwa na hali ya giza wakati Masihi atakufa.**

‘‘Katika siku ile,’’ asema BWANA Mwenyezi, ‘‘Nitalifanya jua litue alasiri na kuifanya dunia iwe giza wakati wa mchana mwangavu” (Amosi 8:9).

**Kutimia**

“*Ilikuwa kama saa sita mchana, kukawa na giza katika nchi yote mpaka saa tisa, kwa sababu jua liliacha kutoa nuru. Pazia la hekalu kwa sababu jua liliacha kutoa nuru. Pazia la hekalu likachanika vipande viwili*” (Luka 23:44, 45).



Reproduction, resale or internet posting prohibited

---

**Unabii wa BibliaArobainina Tisa**
**Masihi atazikwa kwenye makaburi ya matajiri.**

“*Wakamfanyia kaburi pamoja na waovu, pamoja na matajiri katika kifo chake, ingawa hakutenda jeuri, wala hapakuwa na hila kinywani mwake*” (Isaya 53:9).

**Kutimia**



“*Ilipofika jioni, alifika mtu mmoja tajiri kutoka Arimathea aitwaye Yosefu, ambaye pia alikuwa mwanafunzi wa Yesu. Akamwendea Pilato, kumwomba mwili wa Yesu. Pilato akaamuru apewe. Yosefu akauchukua mwili Yesu, akauviringishia nguo ya kitani safi nyeupe na kuuzika kwenye kaburi lake mwenyewe jipya alilokuwa amelichonga kwenye mwamba*” (Mathayo 27:57-60).

**Sehemu ya 5 – Kufufuka kwa Yesu kama vile imenukuliwa katika Maandiko ya Kiyahudi.**

**Unabii wa Biblia wa Hamsini**
**Masihi atafufuka kutoka kwa wafu.**



**"***Nimemweka BWANA mbele yangu daima. Kwa kuwa yupo mkono wangu wa kuume, sitatikiswa. Kwa hiyo moyo wangu una furaha na ulimi wangu unashangilia, pia mwili wangu utapumzika salama, kwa sababu hutanitelekeza kuzimu wala hutaacha Mtakatifu Wako aone uharibifu. Umenijulisha njia ya uzima, utanijaza furaha katika uwepo wako, pamoja na furaha za milele katika mkono wako wa kuume"* (Zaburi 16:8-11).

**Kutimia**

*"Lakini Mungu alimfufua kutoka kwa wafu akamwondolea uchungu wa mauti, kwa sababu haikuwezekana yeye kushikiliwa na nguvu za mauti. Kwa maana Daudi asema kumhusu yeye: '' 'Nalimwona Bwana mbele yangu siku zote. Kwa sababu yuko mkono wangu wa kuume, sitatikisika. Kwa hiyo moyo wangu unafurahia na ulimi wangu unashangilia, mwili wangu nao utaishi kwa tumaini. Kwa maana hutaniacha kaburini, wala hutamwacha aliye Mtakatifu wako kuona uharibifu. Umenionyesha njia za uzima, utanijaza na furaha mbele zako.'*



*'Ndugu zangu Waisraeli, nataka niwaambie kwa uhakika kwamba baba yetu Daudi alikufa na kuzikwa, nalo kaburi lake lipo hapa mpaka leo. Lakini alikuwa nabii na alijua ya kuwa Mungu alikuwa amemwahidi kwa kiapo kwamba angemweka mmoja wa wazao wake penye kiti chake cha enzi. Daudi akiona mambo yaliyoko mbele, akanena juu ya kufufuka kwa Kristo, kwamba hakuachwa kaburini, wala mwili wake haukuona uharibifu*" (Matendo 2:24-31).

Reproduction, resale or internet posting prohibited

**Yesu yuko hai!**

**Unabii wa Biblia Hamsini na Moja**
**Masihi atazaliwa upya kutoka kifo kama Mwana wa Mungu.**

***"**Nitatangaza amri ya BWANA : yeye aliniambia, "Wewe ni mwanangu, leo nimekuwa Baba yako*" (Zaburi 2:7).

**Kutimia**

*"Nasi tunawaletea habari njema kwamba yale Mungu aliyowaahidi baba zetu sasa ameyatimiza kwetu, sisi watoto wao kwakumfufua Yesu, kama ilivyoandikwa katika Zaburi ya pili, " 'Wewe ni mwanangu, leo nimekuzaa.' Kwa kuwa Mungu alimfufua kutoka kwa wafu asioze kamwe, alitamka maneno haya: " 'Nitakupa wewe baraka takatifu zilizo za hakika nilizomwahidi Daudi.' Kama ilivyosemwa mahali pengine katika Zaburi, "Hutamwacha Mtakatifu wako aone uharibifu" (*Act 13:32-35).

***"**Kwa maana ni malaika yupi ambaye wakati wo wote Mungu alipata kumwambia, "Wewe ni Mwanangu, leo Mimi nimekuzaa*?"(Waebrania 1:5).

**Fumbo lilofunuliwa**. Yesu alifufuka kutoka wafu kama "kiupe kipia" au kiupe ambacho hakijawai kuwepo hapo awali.

*"Kwa hiyo kama mtu akiwa ndani ya Kristo, amekuwa kiumbe kipya, ya kale yamepita, tazama, yamekuwa mapya*" ( 2 Wakorintho 5:7).

Reproduction, resale or internet posting prohibited

---

**Unabii wa Biblia Hamsini na Mbili**
**Masihi atarudi tena mbinguni kwa Mungu.**

***"**Ulipopanda juu, uliteka mateka, ulipokea vipawa kutoka kwa wanadamu, hata kutoka kwa wale walioasi, Ee BWANA, ili wewe upate kuishi huko*" (Zaburi 68:18).

**Kutimia**

*"Akiisha kuwaongoza mpaka kwenye viunga vya Bethania, akainua mikono Yake juu na kuwabariki. Alipokuwa anawabariki, akawaacha, akachukuliwa mbinguni"* (Luka 24:50-51).

**Unabii wa Biblia Hamsini na Tatu**

**Messaya ataketi mkono wa kuria wa Mungu katika kiti cha enzi.**

"*BWANA amwambia Bwana wangu: "Keti mkono wangu wa kuume, mpaka niwafanye adui zako kuwa mahali pa kuweka miguu yako''* (Zaburi 110:1).

**Kutimia**

*"Basi, kwa kuwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu, Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu*" (Wakolosai 3:1)

***"***Mwana ni mng'ao wa utukufu wa Mungu na mfano halisi wa nafsi Yake, akivihifadhi vitu vyote kwa neno Lake lenye uweza. Akiisha kufanya utakaso kwa ajili ya dhambi aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko mbinguni*" (Waebrania 1:3).

*"Mungu alimtukuza akamweka mkono wake wa kuume kuwa kiongozi na Mwokozi ili awape Israeli toba na msamaha wa dhambi" (*Matendo 5:31).

Reproduction, resale or internet posting prohibited

### Sehemu ya 6 – Muhtasari wa Unabii wa Masihi.

### Unabii wa Masihi kwa muhtasari
### Unabii kuhusu Yesu

Kuna zaidi ya unabii 300 yule Yesu alitimiza wakati wa kuzaliwa kwake, maisha kifo na kufufuka kwake, lakini tazama kama mfano tu kumi na saba wale walikuwa mashuhuri.

Welekeo ulio kusanywa kinyume na hawa kumi na saba ilitabiriwa inakuwa imeteshana ama imelingana na nafasai moja ndani ya:

480,000,000,000,000,000,000,000,000,000,000,000. (480 billioni x 1 billion x 1 Trillioni).

Katika maisha yake Yesu Kristo mwenyewe kuna zaidi ya unabii 3000 uliweza kutimiza. Ni ya dhikika kuwaza ya kwamba haya yote unabii itatimizwa na mtu mmoja. Tukiwa nafasi moja kwa habari iliyofuatwa na sufuri 1818! Kukupa wewe wazo la ukubwa wa hii jamba fikiri juu ya mpira uliywekwa na eletriniki (million billion, mbili na nusu humaliza mstari mmoja ukiwa na kipimo tafakari kupanua kwa kiwango cha ulimwengu umekuwa miaka ya mwangaza billion nne katika kiepnyo (mwaka wa mwangaza ukiwa umbali ambao mwangaza hutembea katika mwendo wa zaidi ya maili 186,000 kwa sekudi.

Zidisha hii kwa quadrillion 600. Kutoka kwa kikapu cha eletroniki,toa eletrioniki moja na "uipake"rangi nyekudu na uirudishe kwa kikapu na vizungushe pamoja na zingine kwa miaka mia. Pumba za mwanadamu na utume achukue atoe wakati wa kwanza.

**Haiwezekani**? Kwa wakati sawa, Kristo aliishi na kufa kulingana na maandiko "ajali" haiwezekani?kwa wakati sawa, Yesu Kristo aliishi na kufa na kufufuka, ns sasa anaishi kulingana na maandiko na haya yote kwa "ajali"[2]

*Isaya 42:9 inasema, "Tazama, mambo ya kwanza yametokea, nami natangaza mambo mapya, kabla hayajatokea nawatangazia habari zake*

Reproduction, resale or internet posting prohibited

[2] Pratney, Winkie, kitabu cha *WAFUASI WA YESU (FOLLOWERS OF JESUS*) – Bethany House Publishers, Minneapolis, MN. 1977 uk. 72.

## Sehemu ya 7 - Unabii wa Kihistoria

### Unabii wa Biblia wa Hamsini na Nne
### Unabii kuhusu mji wa Yeriko[3]

**"***Wakati ule Yoshua akatamka kiapo hiki akasema, "Alaaniwe mbele za BWANA mtu atakayeinuka kuujenga tena mji huu wa Yeriko, "Kwa gharama ya mzaliwa wake wa kwanza wa kiume ataweka misingi yake, kwa gharama ya mtoto wake wa mwisho ataweka malango yake*.'' (Joshua 6:26)

**Kutimia**

Joshua 6:26 iliandikwa wakati 1380 BC. Huu unabii ulitabiriwa haswa kabisa.

1. Jiji la Jeriko litajengwa
Lilitimizwa wakati mfalme Ahabu alikuwa na Hiel akajenga.

2. Wakati wale waujenga waliweka msingi wa Jeriko mwana wake atakufa.
Lilitimizwa wakati mwanaye Hiel wa Abiramu alikufa.

3. Wakati wajeunga waliweka lango zajiji mtoto wake mdogo atakufa.
Lilitimizwa wakati mtoto wake mdogo Hiel alikufa (1 Wafalme 10:34).

Reproduction, resale or internet posting prohibited

---

### Unabii wa Hamsini na Tano wa Biblia
### Unabii wa Danieli kuhusu kuja kwa Masihi Yerusalemu.

Jambo moja la kushangaza la Unabii katika neno lake Mungu ni unabii wa Danieli sura ya 9 kusema ile siku haswa Yesu atakapo ingia. Yerusalemu kusulubishwa miaka **500 nyumaye ndio ifanyike!**



Danieli alikuwa maeonyeshwa unabii mwingi katika maono sura ya 9 imeandikwa malaika Gabrieli kuja kwa Danieli na kusema unabii wa kushangaza sana kwake.]aliwambia watu wa Mungu watakuwa na kipindi cha wiki 70 kama wamesahaulika kwa historia, kwa huu muda mambo kaddhaa yatatendeka.

---

[3] Wayne Mckellips – haki miliki 1996, 1999, 2000. http://www.trustthebible.com/prophecy.htm

Wiki ya 69 kwa 70 imeweza kutimizwa kwa kihistoria kuna kunyamaza miaka elfu na tena wiki ya mwisho itatimizwa. Hii ni jambo la kawaida kwa unabii wa Biblia. Katika njia za kiroho tuko wiki ya mwisho kwa maisha yetu sasa.

Neno wiki ni "shabua" lilikuwa Kiebrania inamaanisha saba, ni kama kusema dazani. Agano la kale lote linadhibitisha hii shikanishwa na miaka (Walawi 25).

Danieli alifikiri kwa kipindi cha miaka saba kwa kila "wiki".

Tutaenenda kutazamia wiki ya 69 ile sasa ni historia na unabii uliotimizwa kwa njia ya kiungu.

Mwaka katika agano la kale haukuwa na siku 365 lakini siku 360; imedhibitishwa katika mwanzo 7:11-8:3. Inaelezea gharika lilika siku 150 na tena inatupa sisi kipindi cha miezi tano.

Mwanzo wa tokeo la huu unabii ni kujadiliwa kwa himizo la kulijenga tena Yerusalemu, mpaka njia ukuta na handaki la maji kama kizuizi kinyume na adaui zao. (Danieli 9:25).

Mwanzo ilikuwa kuweka himizo kujenga tena jiji nah ii ilipeanwa katika Nehemia 2:1. Ilikuwa mwezi wa Nisan mwaka wa 20, mwaka wa mfalme Artaxerxes. Alianza kutawala katika 465 BC + maika 20 = 445 BC kwa hivyo amri ilitendeka katika 445 BC mwezi wa Nisan 445 BC Nisan= Machi 14,

69 wiki x 7 x siku 360 = siku 173,880

**Sasa kwa hisabati zingine.**

**Kutimia**

Ongeza kwa Machi,14 445 BC siku 173,880 = Aprili 6, 32AD na ni siku ile haswa Yesu aliingia Yerusalemu akiwa juu ya punda kwa uingizo wa ushindi. Ni unabii wa kushangaza aje na timizo!

Reproduction, resale or internet posting prohibited

---

**Unabii wa Biblia wa Hamsini na Sita**

**Moja za unabii wa kushangaza iliyotolewa na Ezekiel.**

Ilikuwa msemo wa kila mwezi (inaweza kuwa hata sasa) Wanana wa kurudi kwa Wana Waisraeli kwa nchi yao ya ahadi, baada ya kutokuwa kwa zaidi ya miaka 1900. Mwaka ulikuwa 1948!

Katika 70 AD kidogo miaka baaya ya kufufuka kwake Yesu, mkuu wa Kirumi Titus alikuja na kuharibu Yerusalemu wayahudi walitawanywa kote ulimwenguni starabu mwingi ulikuja Israeli kuiba lake Mungu. Nyumaye katika 1940's Hilter akajaribu kuharibu kuwepo kwa Waisraeli katika ulimwengu.

Ni jamii hii tu ya watu iliweza kuendelea kuishi miaka elfu bila nchi.

Katika 1948 (wakati wa maisha yangu) baada ya vita vya pili vya dunia na mwanguko wa Hitler, Wayahudi wakaja pamoja na kufanya kuwa nchi mpya inayoitwa Israeli. Nilioa kwa Televisheni! Niliona muungano wa mataifa ukipigia kura kuwa nah ii.

**Ezekieli alipewa hii unabii kwa njia isiyo ya kawaida kutoka kwake Mungu.**

**"***Kisha chukua bamba la chuma, ukalisimamishe liwe kama ukuta wa chuma kati yako na huo mji, nawe uuelekeze uso wako. Huo mji utakuwa katika hali ya kuzingirwa, nawe utauzingira. Hii itakuwa ishara kwa nyumba ya Israeli.*

*"Kisha ulale kwa upande wako wa kushoto na uweke dhambi za nyumba ya Israeli juu yake. Utazibeba dhambi zao kwa idadi ya siku utakazolala kwa huo upande mmoja.*

*Nimekupangia idadi ya siku kama miaka ya dhambi yao. Kwa hiyo kwa siku 390 utabeba dhambi za nyumba ya Israeli.*

*"Baada ya kumaliza hili, lala chini tena, wakati huu ulale chini kwa upande wa kuume, uchukue dhambi za nyumba ya Yuda.* (Ezekieli 4:3-6).

Mungu alisema hii itakuwa ishara kwa Waisraeli alimwambia Ezekieli alalie wake wa kushoto siku 390 ( ikisimamia miaka 390) na tena alale upande wa kulia kwa siku 40 (ikisimamia miaka 40). Yote ikawa miaka 430. Hii itakuwa ishara ya kwamba adhabu yao itakuwa ya miaka 430.

Nyakati za 536 BC waliachiliwa kutoka Babiloni. Ukihesabu miaka 70 ya utumwa huko Babiloni, walikuwa bado miaka 360 imebaki (430-70) =360.

lIhali hakuna lililo tendeka mwisho wa kipindi cha miaka 360. Wengi wa Wayahudi walikuwa bado Babiloni, sasa inajulikana kama Iraq na Iran, na walikuwa wamerudi nyuma tu. Walikataa kutbu dhambi kwa kutotii kwao.

Suruhu la hii fumbo iko katika Walawi 26 pale inaelezea ya kwamba adhabu ya Waisraeli inategemea na kutii na kutotii kwa amri zake. Mungu alisema ya kwamba ikiwa Wana Waisraeli hawatatubu adhabu yao itaongezwa kwa 7[4].

Hii inamaanisha miaka 360 ya adhabu iliyotabiriwa na Ezekieli iliongezwa na 7 (360 x 7= 2,520 miaka ya Biblia. Mwaka wa Biblia ulikuwa siku 360. kubadili kwa kalenda zetu hiyo itakuwa 2,483.8 miaka (2,520x360=siku 907, 200/miaka 365.25=2,483.8).

Reproduction, resale or internet posting prohibited

**Kutimia**

| | |
|---|---|
| Kuisha kwa utumwa wa Babiloni ulikuwa: | **536BC** |
| Kuongeza | **2,483.8** Siku za kalenda |
| Inakuwa | **1,947.4.** |
| Weka kwa miaka sufuri:<br>Baina ya 1 BC na AD 1 | 1 |
| Kwa hivyo utumwa wa wana wa Israeli utaisha | **Mei1948 .** |

**Na hii ndio siku ile Israeli ilikuja kuwa nchi, Mei 14, 1948.**

[4] Grant Jeffreys, The Signature of God {Sahihi ya Mungu ukurasa 167} (Toronto, Ontario: Frontier Reseach Publications, Inc. 1996)

**Hii ni dhibitisho tosha ya kwamba Mungu ndiye Mwandishi wa Biblia.**

Unabii kama huu kutimia kwa njia kama hii ni zaidi ya kufinyiliwa kwa kwa mwanadamu.Tena inaonyesha kwamba Israeli ni sehemu ya mpango wake Mungu na eti tunaishi siku za kispesheli ; wengine waziita siku za mwisho. Hatujui wakati kila kitu kitafanyika, lakini twajua ya kwamba jambo la Biblia la kihistoria liliweza kufanyika.

---

## Unabii wa Hamsini na Saba wa Biblia;
## Unabii Uliotimia: Dhibitisho la kutegemea Biblia na Hugh Ross, Ph.D.[5]

Miongoni mwa vitabu zote zimeweza kuandikwa Biblia ni ya kipekee na hutabiri mambo haswa kwa –udani – miaka mingi , wakati mwingine kwa karne kabla ije kutendeka karibu unabii. 2500 umeonekana katika makaratasi ya Biblia, kama 2,000imeweza kutimika kabisa bila makosa.

(Yaliyo baki 500tunapo karibia siku za mwisho itaonekana kujifungua kama siku zitakapo kuwa zikiendelea).kwa kuwa uwezekano wa kila moja ya hizi unabii kuwa zimetimizwa kwa nafasi ya kiwango chini kuliko moja kwa kumi (umbo la kushikilia kale)na kutoka unabii kunazo sehemu za kutegemea moja na mwingine kinyume kwa unabii wote umeweza kutimizwa kwa nafasi bila makosa chini ya moja kwa 102000(Hiyo ni 1 ikiwa na 2000 sufuri (kuandika nyumba)!

Mungu si yeye pekee, ilhali mwenye hutumia mambo ya baadaye kupata umakini wa watu.Shetani hata yeye hufanya hivyo. Kupitia dairvoyants(Kama Jeanne Dixon na Edgar Cayce)Maroho ya kishetani na wengine huja kutabiri wa kwa maana, hata kama ni chache ikiwa na wingi kama asilimia sitini hakika, haiwezi kuwa kamili kabisa.Misemo kutoka kwa shetani, kuendelea, hukosa kulingana na maelezo ya unabii wa Biblia, tena haina mwito wa kutubu.

Reproduction, resale or internet posting prohibited

Mtihani wa acid wa kutabua nabii wa Mungu imeweza kuandikwa na Musa katika Kumbukumbu 18:21-22.Kulingana na vipengele za Biblia (na zingine),Nabii wa Mungu kutokana na mnenaji wa kishetani ni asilimia 100 utabiri wao na hakuna nafasi ya makosa.

Kama uchumi huruhusu maelezeo yote ya unabii wa Biblia kwamba umeweza kutimilika ile inafuatia kwa mazungumuzo ya hatua ya juu iliyofupishwa,kiwango cha mradi na nguvu za uumbaji zinaelezea matokeo. Wasomaji wanahimizwa kuchangua wengi na kufanya utafiti kuhusu historia yao.

(1)Nabii Isaya alitabiri kuhusu mshindi aliyeitwa Cyrus ataharibu Babiloni na kushinda wa Msiri .Pamoja na wengi walio julikana ulimwengu. Isaya akasema, atafikiri kuleta wayahudi na kuwaweka huru bila malipo yeyote (Isaya 44:28, 45:1na 45:13). Isaya alitabiri miaka 150 mbele ya Cyrus kuzaliwa miaka 180 mbele Cyrus alitenda moja ya hizi na akafanya hatimaye akafanya yote na mbele miaka 80 kabla ya uhamisho wa Wayahudi.

(Uwezekano wa nafasi ya kutimiza =kwa 1015).

---

[5] http://www.reasons.org/

